JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

Simu: +255 22-2928132
Fax: +25522-2928137
Baruapepe: temeke@temekemc.go.tz
Tovuti: http//.www.temekemc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi
92 Barabara ya mandela/Taifa,
15833 - **DAR ES SALAAM,**
S.L.P: 46343
TANZANIA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MAFANIKIO KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI MBALIMBALI KWA ROBO YA PILI NA MIPANGO YA UTEKELEZAJI KWA MIRADI INAYOENDELEA KUTEKELEZWA

Temeke, Dar es Salaam, March 02, 2023.

Halmashauri ya manispaa ya Temeke inasimamia utekelezaji wa majukumu mbalimbali chini ya wizara ya OR - **TAMISEMI** na ilani ya Chama Cha Mapinduzi (**CCM**), moja ya majukumu hayo ni kuhakikisha Wananchi wanapata huduma stahiki na kwa kiwango bora, katika upande huo (wa utoaji huduma) manispaa ya Temeke imefanikiwa.

Katika robo ya kwanza na ya pili ya mwaka wa fedha **2022/2023** Halmashauri ya manispaa ya Temeke imefanikiwa kutekeleza miradi iliyokuwa kwenye mipango na ile iliyotokana na maelekezo ya Serikali Kuu, lengo hasa likiwa ni kuwapatia Wananchi huduma bora kama dhima ya Manispaa inavyojieleza.

Kwa kuzingatia vipaumbele vya Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, manispaa ya Temeke imeendelea kuboresha miundombinu ya elimu ambapo imetoa kiasi cha shilingi za Kitanzania bilioni 1(1,000,000,000) katika mapato yake ya ndani kuongezea katika fedha zilizoletwa na serikali kuu ili kujenga madarasa ya ghorofa katika shule za sekondari Lumo pamoja na Dovya huku kila gorofa likiwa na vyumba vya madarasa 32 .

Ifahamike kuwa ujenzi wa madarasa hayo ya ghorofa, ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa **207**, ujenzi ambao unatekelezwa kwa fedha kutoka serikali kuu ambapo Manispaa ilipokea kiasi cha shillingi bilioni 4.1. Katika kutekeleza mradi huo Manispaa ilizingatia uhaba wa maeneo ambao umetokana na wingi wa watu na shughuli za kibinadamu hasa makazi na biashara, ikaamua kutoa kiasi hicho cha fedha (Bilioni 1) ili kuwezesha ujenzi madarasa hayo ya ghorofa katika shule za sekondari Lumo na Dovya**.** Ujenzi unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwishoni wa mwezi March 2023.

Kupitia ujenzi wa vyumba vya madarasa 207, shule ya sekondari Lumo imefanikiwa kupata vyumba vya madarasa **56**, vyumba hivyo vitaondoa changamoto ya uhaba wa vyumba vya madarasa iliyokuwepo kutokana na kupokea wanafunzi kutoka takribani shule **6** mpaka **7**, sambamba na kuondoa adha ya wanafunzi kusafiri umbali mrefu kufuata shule zilipo hivyo kupunguza usumbufu na gharama za usafiri kwa Wazazi.

Ujenzi wa shule ya ghorofa katika shule ya Sekondari Dovya utasaidia kupunguza mrundikano wa wanafunzi katika shule za Sekondari zilizopo katika kata ya Chamazi ambapo shule ya sekondari Chamazi kwa mwaka 2022 pekee ina jumla ya wanafunzi **3246**, shule ya sekondari Mbande ina jumla ya wanafunzi **3039**, Saku **2470**, na shule ya sekondari Dovya kwa mwaka uliopita ilipangiwa wanafunzi **450** na wote waliingia darasani, hivyo ujenzi wa shule ya ghorofa utasaidia kupunguza msongamano katika shule hizo.

Utekelezaji wa ujenzi wa maghorofa hayo unafanywa chini ya idara ya ujenzi, na utekelezaji upo katika hatua za mwanzo.

Manispaa ya Temeke kwa kutambua idadi ya Wanafunzi na uhaba wa madarasa imejipanga kujenga jengo la ghorofa katika shule ya msingi Buza, ambayo ina jumla ya wanafunzi **4406** (kwa darasa la kwanza hadi la saba) na wanafunzi **109** kwa darasa la awali ambapo kwa uandikishaji wa mwaka wa masomo 2022/20223 jumla ya wanafunzi **612** wameandikishwa (wanafunzi **62** kwa elimu ya awali na **560** kwa darasa la kwanza).

Shule ya msingi Buza ina jumla ya vyumba vya madarasa **31,** inakabiliwa na uhaba wa vyumba vya madarasa **68** ambapo ili kumaliza kabisa tatizo madarasa **99** yanahitajika, kwa uhalisia, ujenzi wa ghorofa utasaidia kupata idadi hiyo ya madarasa kutokana na uhaba wa ardhi uliopo na katika kutii agizo la Serikali kutumia vizuri ardhi iliyopo kwa kujenga majengo ya ghorofa.

Aidha manispaa ya Temeke kupitia idara ya elimu, inatekeleza ujenzi wa shule chini ya mradi wa kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari (SEQUIP) 'Secondary Education Quality Improvement Project' ambapo shule 1 mpya imejengwa katika kata ya Chamazi, mtaa wa Dovya. Majengo yote muhimu kwa uendeshaji wa shule ikiwemo maabara ya kompyuta **01**, Maabara za sayansi **03**, maktaba **01** jengo la utawala **01**, vyumba vya madarasa **08**, matundu **16** ya vyoo, yako katika hatua ya umaliziaji . Mradi huu umegharimu shilingi za Kitanzania **milioni 470 (470,000,000.00).**

Dhima ya utekelezaji wa mradi wa **SEQUIP** ni kutoa fursa ya elimu kwa watu wazima hususani wasichana waliokosa elimu kupitia mfumo rasmi kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ujauzito, umasikini na kadhalika, ili kuongeza ufikiwaji wa wasichana walioshindwa kuendelea na elimu ya sekondari ambapo mradi unalenga kuwafikia wasichana wenye umri kuanzia **miaka 13-20**.

Kupitia idara ya **maendeleo ya jamii** manispaa ya Temeke kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imeafanikiwa kukopesha jumla ya shilingi za Kitanzania **bilioni 3.1** kwa **vikundi 222** ambavyo pia vinafanya marejesho ya ya kila mwezi, fedha zinazorejeshwa zinasaidia kukopesha kwa vikundi vingine zaidi vinavyokidhi vigezo.

Manispaa ya Temeke inaendelea kupokea marejesho kutoka kwa vikundi chechefu ambapo kwa kutumia utaratibu wa ujazaji wa fomu ya makubaliano maalum wadaiwa wanakubaliana kulipa kiasi cha fedha kwa kila wiki au kipindi fulani mpaka deni litakapomalizika.

Aidha manispaa ya Temeke kupitia idara ya maendeleo ya jamii imepokea maboresho ya mfumo wa utoaji mikopo kidijitali ambapo kila muombaji katika kikundi anapaswa

kujisajili katika mfumo kwa kujumuisha namba ya NIDA na kuhakikiwa, hii inasaidia kuboresha utoaji na urejeshaji mikopo kirahisi kwa kuwa na taarifa kamili za mwombaji na mahali anapopatikana.

Jitihada zote hizi zinafanikishwa kwa ushirikiano uliopo baina ya Serikali kuu, manispaa ya Temeke na Wananchi ambao ndio walipa kodi. Ushirikiano huu ndio unaopunguza kiwango cha umasikini katika jamii zetu, sambamba na kuboresha upatikanaji wa huduma muhimu za Kijamii.

Kupitia **idara ya afya** manispaa ya Temeke imefanikiwa kuboresha upatikanaji wa huduma hususani kwa watoto kupitia kampeni mbalimbali za afya ambapo jumla ya watoto **481,272** wamepatiwa chanjo ya Polio. Manispaa ya Temeke inaendelea na utoaji wa chanjo ya Uviko19 ambapo mpaka Februari 28,2023 watu 902,981 wamechanjwa. Pia utoaji wa kingatiba kwa magonjwa ya minyoo, matende na mabusha, utoaji wa vitamini A na kadhalika umefanyika kwa mafanikio makubwa kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo kupita nyumba kwa nyumba.

Kadhalika idara ya afya manispaa ya Temeke imefanikiwa kusogeza huduma kwa Wananchi kupitia kampeni za uelimishaji na upimaji afya (**Afya Check**) kwa kutumia matamasha na sikukuu za kitaifa kama vile Uhuru, siku ya UKIMWI Duniani, siku ya magonjwa yasiyoambukiza na kadhalika ambapo huduma za uelimishaji na upimaji wa magonjwa kama kisukari, presha, saratani mbalimbali, virusi vya UKIMWI, magonjwa ya macho, afya ya akili na elimu ya lishe zilitolewa kwa Wananchi bila malipo katika kituo cha afya Yombo Vituka (Malawi), ofisi za manispaa ya Temeke na viwanja vya Zakhem (Mbagala Rangitatu).
Pia Idara hii imefanikiwa kuongeza idadi ya watumishi wa ajira za kudumu na ajira za mkataba ili kusaidia upatikanaji wa huduma kwa Wananchi kwa kuzingatia muda, ufanisi kazini na uharaka.

Vilevile kupitia Idara ya Afya, Manispaa imefanikiwa kutekeleza masuala mbalimbali ya lishe ikiwemo kusainisha mikataba ya utendaji kazi ya lishe kwa ngazi ya kata na mitaa ili kuweka usimamizi wa afua za lishe zitakazoleta matokeo makubwa kutokana na

kuwekwa misingi ya ufuatiliaji kuanzia ngazi ya chini (Serikali za mitaa) kama yalivyo maagizo ya Serikali.

Kupitia **idara ya ardhi** Manispaa ya Temeke imefanikiwa kusuluhisha mgogoro uliodumu kwa takribani miaka **15,** mgogoro ambao unahusisha fidia ya kupatiwa ardhi nyingine baada ya manispaa ya Temeke kutwaa maeneo ya Wananchi husika kwa ajili ya shughuli za maendeleo ikiwemo ujenzi wa shule, ambapo wananchi **72** wamepatiwa ardhi mbadala katika eneo la **Tungwi Songani** manispaa ya Kigamboni. Viwanja hivyo vilivyonunuliwa na manispaa ya Temeke kwa mapato yake ya ndani, vimethaminiwa na kuthibitishwa na wataalamu wa ardhi kuwa vinafaa kwa matumizi ya makazi na tayari mikataba imendaliwa na itakabidhiwa hivi karibuni.

Licha ya mafanikio yaliyopatikana, manispaa ya Temeke inaendelea kutoa elimu na kuhamasisha walipa kodi kuhakikisha wanakuwa na uelewa na uwajibikaji katika kutekeleza wajibu wao wa kisheria ili kuendelea kuboresha utoaji wa huduma. Manispaa imekuwa ikitumia mbinu mbalimbali ikiwemo matangazo kwa Umma (**Public Addressing**) na ufafanuzi kwa kodi na tozo zinazotakiwa kulipwa pamoja na utaratibu wake, elimu inayotolewa mara kwa mara na wataalam ili kuwajengea Wananchi uelewa juu ya kodi na tozo za Manispaa.
Kwa ushirikiano, kama ilivyo sasa, manispaa ya Temeke inahakikisha ukusanyaji wa mapato unaendelea kuwa nguzo kuu ya mafanikio katika ukamilishaji wa miradi ya maendeleo kwa manufaa ya Wanatemeke.

IMETOLEWA NA:



FRANCISCA F. MSELEMO
KAIMU MKUU WA KITENGO CHA WAWASILIANO SERIKALINI
MANISPAAA YA TEMEKE